

NIPO TAYARI! TOLEO LA DHARURA*

Utangulizi: Dharura yaweza kutokea wakati wowote na pasipo taarifa. Kila mtu katika kaya yenu anaweza kuwa na mahitaji ya kinafsi ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili aweze kujiandaa sawasawa kukabiliana na dharura. Fikiria jinsi mambo kama vile umri, ulemavu, jinsia, hali ya kiafya, mahitaji ya lugha, nakadhalika, yanaweza kuathiri jinsi watu wanavyohitaji kujiandaa kukabiliana katika hali za dharura. Unda matukio 4 tofauti ya hatari ili kuonyesha utayari na mahitaji tofauti ya mwitikio kwa watu.

Shughuli za Kupunguza Hatari Ya Maafa

Muda

Saa 1

Ugumu

Rahisi-Wastani

Rasilimali

Ubao, viweka alama, kalamu

*Shughuli hii imetengenezwa kama muendelezo wa kujifunza unaohusiana na [Pils Web](#) Mradi wa Limitless.

● Hatua ya 1

Tengeneza matukio ya hatari 4 tofauti ya watu katika dharura zinazowezekana.

- Jaribu kufikiri kuhusu dharura zinazoweza kutokea katika maisha ya kila siku. Ni hatari gani inaweza kutokea ufukweni, mlimani, mjini, shuleni, na kadhalika?
- Jumuisha wahusika wenye mahitaji tofauti:
 - Makundi ya kikabila, umri, jinsia, ulemavu, na kadhalika.
- Fikiria ni rasilimali zipi zingehitajika katika hali tofauti za hatari.

● Hatua ya 2

- Ongeza viputo vya usemi kwa kila tukio kutoka kwa mtazamo wa watu wanaozingatia mahitaji yao binafsi. Fikiria juu ya:
 - Nini kilitokea?
 - Nahitaji nini?
 - Najibuje?

